



HeartKids

Kuelekeza utambuzi

Taarifa kwa wazazi au walezi ambao wamepokea hivi karibuni utambuzi mpya kwa mtoto wao.

Kujifunza kwa mara ya kwanza kwamba mtoto wako ana hali ya moyo kunaweza kusababisha hisia mbalimbali.

Inaweza kukusababisha uhisi kuzidiwa. Ni muhimu kukumbuka wewe sio peke yako. Ugonjwa wa moyo wa utoto ni kawaida, na ukali wa kila kesi hutofautiana. Siku hizi, kuna chaguzi nzuri za tiba zinazopatikana kwa aina nyingi za Ugonjwa wa moyo wa utoto.

Ugonjwa wa moyo wa utoto unagunduliwaje?

Kesi nyingi za ugonjwa wa moyo wa utoto zinatambuliwa kabla ya mtoto kuzaliwa, uchunguzi wa ultrasound wakati wa ujauzito. Kesi nyingine zinagunduliwa hivi karibuni baada ya kuzaliwa. Baadhi ya kesi za ugonjwa wa kuzaliwa hazitambuliwi hadi baadaye katika utoto au kwa kesi za adimu, katika utu uzima.

Kesi za ugonjwa wa moyo uliopatikana zinaweza kujitekeza katika utoto kutokana na ugonjwa au maambukizi.



Mtazamo ni nini?

Hakuna tiba ya Ugonjwa wa moyo wa utoto, lakini chaguzi za tiba zinaboreshwawakati wote. Watoto wengi wenye matatizo ya moyo wanaendelea kuishi maisha marefu na ya kawaida.

Baadhi ya watoto wachanga na watoto wenye Ugonjwa wa moyo wa utoto hawahitaji matibabu yoyote. Baadhi za kesi ni ngumu zaidi na zinaweza kuhitaji matibabu ya kila mara au upasuaji mwingu. Timu yako ya matibabu huamua mtazamo na njia bora ya matibabu. Maamuzi yao hufanywa daima kwa msingi wa mtu binafsi.

95%
ya watoto
wanaozaliwa na
kasoro ya moyo ya
kuzaliwa wataishi
hadi utu uzima.^{1, 2}



Leo kuna watu wazima zaidi kuliko watoto wanaoishi na Ugonjwa wa moyo wa utoto nchini Australia. Hii ni kutokana na maendeleo ya haraka ya matibabu katika kipindi cha miaka 60 iliyopita.

Hisia za kawaida

Utambuzi mpya unaweza kuwa na athari kubwa kwa maisha yako na kwa maisha ya familia yako. Kusikia kwamba mtoto wako ana hali ya moyo kunaweza kuwa ya kukasirisha sana.

Ni kawaida kupata hisia kama vile mshtuko, kukataa, hasira, huzuni na kujitenga. Watu wengine watapata hisia hizi kwa nguvu zaidi, na watu wengine wanaweza kuchukua muda mrefu kutulia kuliko wengine.

Uzoefu wa kila familia wa Ugonjwa wa moyo wa utoto ni pekee. HeartKids inaweza kukusaidia kuelekeza uzoefu wako kwa kasi yako mwenyewe.

Kwa nini hii ilitokea kwetu?

Hili ni swali la kawaida. Unapoambiwa kuwa mtoto wako ana kasoro ya moyo, ni rahisi kushtuka na kutengwa. Ni muhimu kukumbuka wewe sio peke yako.

Kasoro za moyo za kuzaliwa ni kati ya aina za kawaida za kasoro ya kuzaliwa, inayoathiri mtoto 1 kati ya watoto 100. Nchini Australia, inamaanisha karibu watoto wachanga 8 wanazaliwa kila siku na aina yoyote ya kasoro ya moyo ya kuzaliwa.³



Wakati mwininge wazazi wanaweza kuhisi hatia au kufikiri kuwa wanapaswa kulaumiwa kwa hali ya moyo wa mtoto wao. Ingawa ni kawaida kutaka kujua kwa nini hii imetokea, katika kesi nyingi za ugonjwa wa moyo wa kuzaliwa, sababu haijulikani.

KATIKA KESI 8 ZA 10 ZA UGONJWA WA MOYO WA KUZALIWA



**HAKUNA SABABU
INAYOJULIKANA⁵**

Kujiandaa kwa miadi yako ya kwanza ya kadiolojia

Vidokezo:

- **Chukua mtu wa familia au rafiki.** Anaweza kukupa usaidizi katika miadi.
- **Wasiliana na timu ya ustawi wa jamii.** Uliza hospitali jinsi ya kuwasiliana na timu yao ya wafanyakazi wa ustawi wa jamii ili kupata usaidizi ziada.
- **Tumia muda kadhaa kufikiria juu ya kile unachotaka kuuliza.** Andika maswali yako ili unaweza kuyakumbuka wakati wa miadi.
- **Andika madokezo.** Andika habari muhimu ili unaweza kukumbuka kile kilichozungumzwa. Unapaswa pia kuandika majina na habari ya mawasiliano ya wataalamu wa afya ulioongea nao.
- **Uliza kwa taarifa kuchukua nawe nyumbani.** Kunaweza kuwa michoro au karatasi za ukweli ambazo unaweza kuchukua nawe nyumbani kwa habari zaidi.

Mawazo ya maswali ya kuuliza:

- Je, hali ya moyo ya mtoto wangu inaitwaje? Je, hali hiyo inaathiri vipi kazi za kawaida za moyo wake?
- Je, ninahitaji kuchukua tahadhari yoyote ya ziada wakati wa ujauzito?
- Nini itatokea wakati mtoto wangu anapozaliwa?
- Mtoto wangu atahitaji matibabu gani? Je, mtoto wangu atahitaji upasuaji?
- Ni mtazamo au ubashiri gani wa muda mrefu?

Mahali pa kupata habari zaidi na usaidizi

HeartKids



heartkids.org.au

Pata maelezo zaidi kuhusu Ugonjwa wa moyo wa utoto na usaidizi HeartKids inaoweza kukupa.



1800 432 785

Piga simu kwa Simu ya msada ya HeartKids ili kupata usaidizi, ushauri na mwongozo.



@HeartKidsAustralia



@HeartKids

Marejeleo

¹ LE GLOAN, L., MERCIER, L., DORE, A., MARCOTTE, F., IBRAHIM, R., MONGEON, F., ASGAR, A., MIRO, J., POIRIER, N. & KHAIRY, P. (2011). "Recent advances in adult congenital heart disease." *Circulation*. 75: 2287- 2295.

² KHAIRY, P., IONESCU-ITTU, R., MACKIE, A. S., ABRAHAMOWICZ, M., PILOTE, L. & MARELLI, A. (2010). "Changing mortality in congenital heart disease." *Journal of the American College of Cardiology*. 56: 1149- 1157.

³ VAN DER LINDE, D., KONINGS, E., SLAGER, M., WITSENBURG, M., HELBING, W., TAKKENBERG, and J. J. & ROOS-HESSELINK (2011). "Birth prevalence of congenital heart disease world-wide: a systematic review and meta-analysis." *Journal of the American College of Cardiology*. 58: 2241-2247.

⁴ CELERMAJER, D., STRANGE, G., CORDINA, R., SELBIE, L., SHOLLER, G., WINLAW, D., ALPHONSO, N., JUSTO, R., NICHOLAE, M., KASPARIAN, N., WEINTRAUB, R. G., CHEUNG, M., GRIGG, L. E., BRIZARD, C. P., WHEATON, G., DISNEY, P., STEWART, S., BULLOCK, A., RAMSAY, J., GENTLES, T. & D'UDEKEM, Y. (2016). "Congenital Heart Disease Requires a Lifetime Continuum of Care: A call for a Regional Registry." *Heart, Lung and Circulation*. 25(8): 750-754.

⁵ BLUE, G. M., KIRK, E. P., SHOLLER, G. P., HARVEY, R. P. & WINLAW, D. S. (2012). "Winlaw DS. Congenital heart disease: current knowledge about causes and inheritance." *The Medical Journal of Australia* 197: 155- 159.

Karatasi hii ya ukweli ilikaguliwa na kusasishwa na HeartKids katika Machi 2021. Iliidhinishwa na Kamati yetu ya Ushauri wa Kliniki wakati wa kuchapishwa. Taarifa za kliniki zinaweza kubadilika baada ya tarehe hii. Taarifa katika karatasi hii ya ukweli ni ya jumla. Sio mbadala wa ushauri wa kimatibabu kutoka kwa daktari wako. Wakati wote ongea na daktari wako kuhusu mambo yanayoathiri afya yako.

Photo by Aditya Romansa on Unsplash